JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya Simu:
"ARDHI"
Simu: 2 113164
Fax: 2124505
Tafadhali unapojibu taja:

S.L.P 9132,
DAR ES SALAAM.

**Kumb. Na. TP/R/157/39** **29 Agosti, 2008**

Makatibu Tawala (M),
TANZANIA BARA

Wakurugenzi wa Miji, Manispaa na Jiji,
TANZANIA BARA

Wakurugenzi Watendaji (W),
TANZANIA BARA

**Yah: KUZUIA VIBALI VYA MABADILIKO YA MATUMIZI YA MAENEO YA WAZI KWA AJILI YA MATUMIZI MENGINE**

Kanuni za utayarishaji mipango ya kina katika miji zinaelekeza kutenga **maeneo ya wazi (open spaces)** kwa ajili ya michezo na burudani kwa kuzingatia viwango maalum. Maeneo haya hutengwa makusudi kwa ajili ya michezo ya watoto wadogo (**tot lots**), viwanja vya michezo (**playgrounds**), maeneo ya mapumziko (**recreation grounds**) na hifadhi ya ardhi (**conservation grounds**). Shughuli za michezo, burudani, mapumziko na hifadhi ya mazingira katika jamii ni muhimu kwa afya na usalama wa wakazi wake. Kukosekana kwa huduma hizi kwenye maeneo ya makazi kunawalazimisha watoto na vijana kucheza barabarani na penyo za nyumba ambako mara nyingi huzua ajali na ugomvi usio wa lazima. Aidha kutumia maeneo yaliyotengwa kuwa maeneo ya wazi husababisha upungufu wa mzunguko wa hewa safi katika sehemu inayohusika.

Kimsingi, hakuna mchoro wa kina unaotayarishwa bila kuwepo na **maeneo ya wazi** yaliyotengwa kwa makusudio yaliyotajwa. Hata hivyo michoro ya kina iliyopo na hali halisi ardhini ni tofauti kabisa. Maeneo mengi ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya burudani, michezo na hifadhi ya mazingira kwenye

michoro yamebadilishwa matumizi tofauti kabisa na ubunifu wa awali. Ni wazi kuwa maeneo mengi ya wazi yamekuwa yakivamiwa kwa ajili ya maendelezo tofauti na yaliyopangwa bila ya kibali kutoka mamlaka husika. Hata hivyo, baadhi ya mabadiliko yamekuwa yakipata baraka za uongozi na vikao vya Halmashauri za Miji inayohusika na hata mengine kutumwa kwa Waziri kwa ajili ya kuombewa idhini.

Watu wengi huyaona maeneo ya wazi kuwa ni maeneo yasiyo na shughuli na hivyo kushawishika aidha kuyavamia au kuomba kubadilishwa matumizi. Hali ya kutodhibiti uvamizi au kuruhusu mabadiliko ya matumizi ya maeneo yaliyotengwa kuwa ya wazi imefanya miji yetu kukosa maeneo ya wazi yanayotosheleza na badala yake kujengwa majengo ya kuishi na shughuli nyingine. Mtindo huu wa kuruhusu au kukosa udhibiti wa mabadiliko ya matumizi ya maeneo ya wazi usipoangaliwa upya na kwa makini zaidi, kutasababisha kumalizika kabisa kwa maeneo ya wazi mijini. Mnamo Mwaka 2001 Serikali ilitoa agizo la kutangaza maeneo yote yaliyotengwa kuwa ya wazi yasigawiwe kwa matumizi mengine. Agizo hili linaendelea kutumika. Hata hivyo pamoja na kuwepo kwa agizo hilo, bado yanaletwa maombi ya mabadiliko ya matumizi ya maeneo ya wazi, na bado yanaendelea kupokelewa na kukubaliwa na Halmashauri za Miji. Maeneo ya wazi ni maeneo ya umma na **yanapaswa kulindwa na umma kupitia uongozi wa mji husika** na siyo kuyabadili na kuyagawa kwa matumizi mengine.

Kwa kutumia mamlaka niliyopewa chini ya **Sheria ya Mipangomiji Sura ya 8 ya Mwaka 2007** vifungu Na. 5-(2) b na 77-(1) (h) naagiza kuwa kuanzia tarehe ya barua hii ni marufuku kwa Halmashauri yoyote kutoa kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi ya eneo lolote la wazi katika miji Tanzania Bara isipokuwa tu pale mabadiliko hayo kama ni ya lazima sana, na kwa matumizi ya umma. Aidha, kuanzia sasa Wizara hii haitatoa idhini kwa maombi yoyote yanayohusu mabadiliko ya matumizi ya maeneo yaliyotengwa kuwa ya wazi isipokuwa yale maeneo ambayo uongozi wa wilaya na mkoa wamethibitisha kuwa ni kwa matumizi ya umma na ni ya lazima kabisa. Kamati zote za Mipangomiji na Wakurugenzi wote wanaagizwa kutokubali maombi ya mabadiliko ya matumizi ya maeneo ya wazi yasiyolenga matumizi maalum ya kitaifa na manufaa ya umma kwenye maeneo yao.

Kwa nakala ya waraka huu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanaombwa kusadia kusimamia utekelezaji wa agizo hilo.

**Capt. John Z. Chiligati (Mb)**
**WAZIRI**

**Nakala:** Mhe. Celina Kombani (Mb.),
Waziri wa Nchi – TAMISEMI,
**DAR ES SALAAM**

" " Wakuu wote wa Mikoa,
**TANZANIA BARA**

" " Wakuu wote wa Wilaya,
**TANZANIA BARA**